


# Taarifa ya Ofisi Ya Mwenyekiti

Pr. Beatus G. Mlozi

## UTANGULIZI

Taarifa hii ya utendaji kazi ya miaka mitatu ya muhula huu imejumuisha mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

1. Ukuaji kiroho wa washiriki.
2. Uwezo wa kujitegemea: kugawa Conference.
3. Rasilimali Watu.
4. Rasilimali Miongozo - Kufundisha uongozi wa Kikristo.
5. Kusukuma uinjilisti kwa njia zote muhimu.
6. Ukuaji wa Kanisa - Malezi na utunzaji wa washiriki.
7. Rasilimali Fedha - Kutumia mfumo mpya wa Adventist Church Oparating System (ACOS)
8. Kujenga ofisi ya makao makuu ya Conference.
9. Mabadiliko ya taswira ya mitaa na Taasisi za Conference.
10. Huduma za Idara na Taasisi zetu.

## UKUAJI WA KIROHO

Njia zilizotumika katika swala zima la ukuaji kiroho wa waumini wa kanisa katika kuwaandaa kupokea uwezo wa Roho Mtakatifu na waumini kuyatoa maisha yao binafsi kikamilifu kwa Mungu na kumtumikia Bwana kama ifuatavyo:

Kwanza kabisa ni uamsho na matengenezo: kumekuwepo na uamsho wa pekee muhula huu ambao unakua siku kwa siku, waumini kurejea madhabahuni kwa njia ya maombi ya mtu binafsi, maombi ya familia, vikundi vya maombi na Kanisa mahalia kwa ujumla wake. Uamsho umefanyika pia kwa kusoma Neno la Mungu (Biblia) kwa mpango, usomaji wa vitabu vya Roho ya Unabii (Pambano Kuu kitabu cha mwaka 2024-2025), Kesha la Asubuhi, Mwongozo wa shule ya sabato kujifunza Biblia kila Robo, ni pamoja na semina za uamsho na matengenezo zilizofanyika ndani na nje ya Conference.

Masomo maalum ya siku 10 za maombi kila mwanzo wa mwaka yalifanyika makanisani pamoja na masomo ya juma la maombi yaliyoandaliwa na kila idara yalifanyika katika makanisa mahalia sawa na ratiba ilivyopangwa kila mwaka.

Pili, kuwafikia wengine. Huduma ya uamsho na matengenezo ndo uhai wa maisha ya mkristo kiroho katika swala zima la utume. Kurejea madhabahuni na kuishi Neno la Mungu na kwenda popote Roho Mtakatifu anapo tuongoza, kwa mwitikio huu tumeweza kufikia familia zingine,

marafiki, majirani, wanafunzi, wafanyakazi wenzetu na watu tunamoishi nao kuwafanya kuwa wafuasi wa Yesu Kristo.

## KUGAWANYWA KWA CONFERENCE

### *Eneo la Kazi Kabla ya Kugawanywa Conference.*

South Nyanza Conference imekuwa ikihudumia mikoa miwili; Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Mwanza ukiondoa Wilaya ya Ukerewe na Sengerema. Eneo la utume limekuwa na takribani ya wakazi **4,614,029** kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022. Hivyo kufanya uwiano wa mshiriki kwa wakazi kuwa mshiriki **1** kwa wakazi **22**.




*Picha 1: Ramani ya Eneo la Kazi la South Nyanza Conference kabla ya kugawanywa.*


Tunamshukuru Mungu kwa kazi kubwa ya utume iliyofanyika tangu tulipozaa Field ya Nyanza Gold Belt Field mwaka 2020, **ni habari njema tena kufikia Mei 13, 2025 Field mpya ya Simiyu River Field (SRF) kuzaliwa.** Eneo la utume la SRF lina Mkoa wa Simiyu na wilaya zake, makao yake makuu yakiwa Bariadi. Bwana atukuzwe kwa mambo makuu aliyotutendea katika Conference yetu.




*Picha 2: Pr. Blasious Ruguri, Mwenyekiti wa Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati akikabidhi cheti cha kupangwa kwa fiel mpya ya Simiyu River Field.*

## *Eneo la Kazi Baada Ya Kugawanywa Kwa Conference.*

Eneo letu la Utume South Nyanza Conference ni Mkoa wa Mwanza kiserikali ukiondoa Wilaya ya Ukerewe na Wilaya ya Sengerema. Eneo hili lina kilometa za mraba zipatazo 7,788 lenye wakazi wapatao 2,473,532 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022. Kanisa letu katika SNC lina washiriki wapatao 90,094 baada ya kugawanywa. Eneo letu la utume lina 3.7% ya waumini wa Kanisa la Waadventista wa Sabato wanaopatika eneo hili, sawa na uwiano wa mshiriki 1 kwa wakazi 27.




*Picha 3: Ramani ya SNC baada ya Conference kugawanywa*

Baada ya kugawanywa kwa Conference May 2025, bado tumeendelea kuwa na maeneo mapya yanayotakiwa kufikiwa kwa kusudi la kupeleka injili. ***“Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa ulimwenguni kote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote, hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.”*** Uelewa kwa waumini wa Kanisa unahitajika kujitolea kwa hali na mali na kutumika kama wamishonari katika maeneo mapya. Roho ya umishonari inahitajika leo kuitikia kaulimbiu isemayo ***Yesu anakuja, Nitakwenda***. Wito kwa Kanisa mahalia, idara, familia, Kundi la vijana na washiriki, watu binafsi watakaojitolea kupeleka injili ya milele kwa kasi wanahitajika sasa, pamoja na wale watakaotoa mali na Karama zao kujenga makanisa maeneo mapya. Nguvu ya umoja kwa uwezo wa Roho Mtakatifu inawezekana.

## RASILIMALI WATU.

Tulianza muhula huu tukiwa na watumishi 372 na kuongezeka kufikia jumla ya watumishi 399 kabla ya kugawa Conference, ongezeko la 7.2%.

## RASILIMALI MIONGOZO:

### *A: Mwongozo na Mwelekeo wa Kanisa Kiutume Toka kwa Viongozi wa Ngazi za Juu.*

Ziara ya Mwenyekiti wa General Conference Dkt., Mch. Ted N. C. Wilson katika Conference yetu mnamo February 2, 2023, alipohutubia waumini wote kupitia Vyombo vya habari toka viwanja vya CCM Kirumba akihimiza swala zima la utume wa Kanisa na kauli mbiu isemay0 “Yesu Anakuja – Jihusishe”; kwamba kila mmoja wetu ni Balozi wa Yesu Kristo, kwa kutambua hili kila mmoja wetu ajihusishe kupeleka ujumbe wa Malaika watatu kwa nguvu.

Feb. 3, 2023 Mwenyekiti wa GC, alitoa semina ya uongozi kwa viongozi na wachungaji waliohudhuria toka Union zote mbili NTUC na STUM katika Kanisa la Waadventista wa Sabato Pasiansi – Mwanza, kuwahimiza kutumika kwa bidii kulihubiri Neno tunapoelekea miisho ya Dunia. Mrs. Nancy Ted Wilson pia, alitoa semina kwa Wenzi wa Wachungaji akiwatia moyo kushikamana na wenzi wao kutumika sawa na wito walioitiwa.



*Picha 4: Mwenyekiti wa GC Dkt. na Mch. Ted N. C Wilson akihutubia waumini wa Kanisa tokea viwanja vya CCM Kirumba – Mwanza*



*Picha 5: Dt. na Mch. Ted Wilson akitoa semina ya uongozi kwa viongozi na wachungaji.*



*Picha 6: Mrs. Nancy Ted Wilson akiwa na wenzi za Wachungaji*

Mwanzoni mwa mwaka 2023 kanisani Nyegezi - Mwanza, maofisana wakurugenzi wote wa Union waliendesha semina wakitoa maelekezo na dira ya Kanisa katika swala zima la utume na utumishi wetu kama wafanyakazi wa Conference.



*Picha 7: Viongozi na Wakurugenzi wa NTUC wakitoa semina elekezi kwa wafanyakazi SNC*

Ziara ya Mwenyekiti wa Union wa NTUC Mch. Mark W. Malekana Juni 23-30, 2024 alitembelea mitaa ya Meatu, Mwanuzi, Mshikamano, Majengo Meatu, Mwandoya, Nkololo, Lamadi, Mwamapalala Itilima na makanisa ya mitaa ya Bariadi Mjini ndani ya Conference yetu.

Dhima mahususi ilikuwa ni kutoa mwongozo na mwelekeo wa Kanisa na utume wake kwa wakati huu, akiwapongeza na kuwatia moyo kuhakikisha kuwa wana endana na mpango wa Kanisa katika kazi ya utume huku akihimiza washiriki kufanya kazi kwa bidii na kurudisha zaka na sadaka kwa uaiminifu; na kuwataka waumini kufanya kazi ya Mungu.  Ni pamoja na kuweka mawe ya msingi kwa makanisa na Shule ya Msingi Kanisa la Mshikamano na kuweka wakfu miradi mbalimbali ya kanisa akisisitiza washiriki kuwa sehemu ya kufanikisha mpango wa Kanisa wa kubadili muoneokano au taswira ya majengo na mazingira kwa ujumla wake (image change).



*Picha 8: Mwenyekiti wa Union ya NTUC, Mch. Mark W. Malekana akihutubia waumini katika ziara yake aliyoifanya mkoani Simiyu.*

Katibu wa Unioni ya NTUC Mch. Magulilo Mwakalonge, alitembelea Taasisi na makanisa akitoa semina kwa wachungaji na watendakazi wa makanisa ambao ni wajumbe wa mabalaza ya Kanisa, akisisitizia swala zima la kulinda umoja wa Kanisa kwa kujitoa kikamilifu kulipenda Kanisa na kulithamini katika kutetea Sera, Kanuni, taratibu na miongozo yote ya Kanisa hili.



*Picha 9: Pr Mwakalonge*

Ni pamoja na Wachungaji 98% toka SNC waliohudhuria semina zilizoendeshwa na Union ya NTUC katika Kanisa la Singida Kati zilizohusu malezi ya kichungaji na kuzingatia ratiba zao za kazi.

*B: Conference kuhusikia kutoa Rasilimali Miongozo (uongozi wa kikristo)*

Viongozi Conference walitoa semina kwa watumishi wote kila mwanzo wa mwaka na kutoa Handbook 48 kwa watumishi wapya na waliohamia.

Semina za uongozi toka Conference zilitolewa kwa wachungaji wa mitaa, wajumbe wa mabaraza ya Kanisa juu ya kulinda umoja wa Kanisa kwa kuongoza na kufanya shughuli zake kufuatisha mifumo, Sera, na Miongozo ya Kanisa. Ikiwa ni matokeo ya semina hizo Miongozo ya Kanisa 1,647 ilinunuliwa na makanisa.

Kupitia program ya Team Work viongozi na Wakurugenzi waliungana kwa pamoja kufikia Kanda na mitaa ya Conference kila mwanzo wa mwaka kati ya mwezi Februari na Machi kuseminisha watendakazi wa Kanisa katika kusisitiza utume na malengo ya Kanisa kwa kila idara na kutoa miongozo ya idara. Semina hizi zilifanikiwa kwa 100% sawa na malengo tuliyojiwekea kufikia mitaa yote 96 na kuleta matokeo mazuri ya kiutendaji SNC.

Wachungaji wamekuwa na semina zilizoendeshwa na uongozi wa Conference kuhusiana na wito wa Mchungaji katika swala zima la utume na semina kwa wachungaji wapya waliojiunga katika huduma ya kichungaji.

Tunatambua semina za wachungaji wa mitaa zinazotolewa kila mwanzo wa mwaka katika makanisa mahalia kuwaandaa watendakazi wa Kanisa kutumika kufikia mipango na malengo ya utume wa kanisa.

## UINJILISTI:

Uinjilisti ni mpango mzima wa kuongeza idadi ya washiriki katika kutekeleza Agizo la utume na kauli mbiu isemayo **“Nitakwenda - Kuwafanya Kuwa Wanafunzi”** (I Will Go - Make Disciples), kwamba kila mshiriki alitakiwa kutimiza agizo la Mathayo 28:19 *“Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi ....”*

### *Mipango Iliyotumika Kuongeza Idadi ya Washiriki:*

Mpango wa kuongeza idadi ya washiriki (Doubling Membership) ulianza mara moja mwanzoni mwa muhula huu, ikiwa sehemu ya program ya *ECD Evangelistic Impact 2025 (EEI)*, iliyozinduliwa rasmi katika Union ya Kaskazini mwa Tanzania (NTUC) tarehe 13/01/2024 jijini Mwanza katika kanisa la Waadventista wa Sabato Kirumba. Mwenyekiti wa Union, Mch. Mark W. Malekana, aliioongoza timu ya Union katika kuwasilisha mkakati huu wa uinjilisti, akihimiza kila mshiriki kuleta mtu mmoja kwa Yesu. Kwa pamoja Viongozi wote, wakurugenzi wote wa idara, wachungaji wote na washiriki wote, waliitikia wito wa kushiriki kikamilifu kwa mpango huu hadi ifikapo mwaka 2025.




*Picha 10: Mch. Mark W. Malekana, Mwenyekiti NTUC akizindua ECD Evangelistic Impact 2025.*

SNC katika kuunga mkono mkakati huu wa ECD Evangelistic Impact 2025, tuliuzindua rasmi katika Conference yetu tarehe 26/01/2024 mkoani Simiyu katika Kanisa la Waadventista wa Sabato Bariadi na Mwenyekiti SNC, Mch. Beatus G. Mlozi; kwa pamoja wakurugenzi, wachungaji, wazee wa makanisa

na washiriki wote walipokea jukumu hilo kuwa mashahidi wa Yesu Kristo na kuweka mipango na mikakati ya kuwafikia watu 71,000 na kuwabatiza ifikapo mwaka 2025.




*Picha 11: Pr. Beatus G. Mlozi akizindua ECD Evangelistic Impact 2025 ya Conference - Bariadi*

### *Matokeo ya Program ya ECD Evangelistic Impact (EEI) 2025*

Tunamshukuru Mungu kwa timu ya Maofisa na Wakurugenzi wote wa Idara Conference, Wachungaji wa mitaa, Wazee wa makanisa, viongozi wa idara makanisani, walei waijilisti wa vitabu na washiriki wa Kanisa katika umoja wa Kanisa kutekeleza agizo la utume **"Enendeni**...." Matokeo ni kama ifuatavyo: -

**Mahubiri ya Net Event:** SNC tulishiriki mahubiri yote yaliyorushwa kupitia vyombo vya habari, nayo ni mahubiri ya Kihonda Net Event, Hope for Africa, Kahama Net Event, na Dar es salaam Net Event jumla ya watu 17,573 walibatizwa. Walei 1047 walishiriki katika mahubiri haya.

**Mahubiri ya hadhara yaliyoandaliwa na Idara katika kutimiza Agizo la utume:** Mahubiri ya Maisha ya Familia, mahubiri ya Kumbuka Nyumbani (Home Coming), Mahubiri ya vijana, mahubiri ya Watoto na mahubiri ya Hope for Big Cities; kwa ujumla wake watu 14,424 walibatizwa.

Pamoja na mahubiri yaliyofanyika hapo juu, idara ya Afya na kiasi, AWM, Uchapaji, Elimu na Taasisi zake, na vitengo vingine vyote walishiriki katika mahubiri ya EEI.




*Picha 12: Mahubiri ya Idara ya Huduma za Familia.*




*Picha 13: Washiriki wakifuatilia mahubiri ya NET Event.*

**Uinjilisti kwa njia ya masomo ya Sauti ya Unabii (Voice of Prophecy)**. Mwenyekiti wa SNC, Mch. Beatusi G. Mlozi alizindua program ya masomo ya Sauti ya Unabii Feb. 2, 2025 kanisani Mabatini, wakiungana kwa pamoja maofisa na Wakurugenzi kufikia mitaa yote ya Conference kuhimiza na kusisitiza **Idara zote, wachungaji wote, wazee wa makanisa yote na kila mshiriki kuhusika kikamilifu katika kumsomesha angalau mtu mmoja kupitia masomo ya Sauti ya Unabii (VOP).** Muitikio wa program hii, masomo ya Sauti ya Unabii 13,978 yalinunuliwa na watu 3,198 walibatizwa.



*Picha 14: Mwenyekiti Pr. Beatusi Mlozi akizindua mpango wa masomo ya Sauti ya Unabii katika Kanisa la Mabatini.*

**Uinjilisti kupitia kitengo cha AMR:** Watumishi Makao makuu ya SNC wakiungana na Kitengo cha AMR kugawa chakula wakati wa Ramadhan ya mwezi April 2023. Katika kutimiza mpango mzima wa ECD Envangelistic Impact 2025, program maalumu iliandaliwa kupitia kitengo cha AMR, ambapo viongozi na watumishi wa makao makuu ya SNC, wanachama wa ATAPE, Vijana pamoja na waumini wa kiislamu tulishiriki pamoja kufanya usafi eneo la soko la Kirumba, ikiwa ni maandalizi ya mahubiri ya Maisha ya Familia kituo cha High Profile, Mwanza Hotel.



**Uinjilisti kupitia Kitengo cha Global Mission katika kutimiza Agizo la Utume:**
Kitengo cha Global Mission kimekuwa kikishughulika na kuingia maeneo mapya ambayo hayajafikiwa na ujumbe wa malaika wa tatu na kufungua makanisa maeneo mapya. Katika Muhula huu kitengo cha Gobal Mission wamefikia maeneo mapya 29 SNC kabla ya kugawanywa. Wamefanikiwa kufungua vituo 5. Wameezeka makanisa 4: Kang'anga - Butimba, Mwangudo - Paji, Kumalizia kuezeka Kanisa la Kona Fela - Kishili ni pamoja na Kanisa la Ibanda - Jiwe Kuu.

Huduma za usafiri wa Pikipiki 7 zilizotolewa kwa waanzilishi wa utume maeneo mapya (Gobal Mission Pioneers) na baadhi ya wachungaji wa mitaa. Biblia 200 zimetolewa kwa waumini wasio na Biblia.



*Jumla ya watu wote waliompokea Yesu Kristo na kubatizwa Muhula huu kwa mujibu wa Takwimu za washiriki SNC kuanzia Robo ya tatu Sept. 2022 hadi kufikia June 2025 ni Watu 55,906.*

## SHEREHE ZA JUBILEE YA MIAKA 150 YA UTUME ULIMWENGUNI
Sherehe za Jubilee kutimiza miaka 150 ya utume wa Kanisa la Waadventista wa Sabato ulimwenguni, katika Conference yetu sherehe hizi zilizofanyika Agosti 22-24, 2024 katika Shule ya Bupandagila Adventist Secondary School; kuenzi wamishionari wa kwanza walioingia usukumani kuleta injili ni pamoja na wazee wetu waliopokea injili na kutumika kwa uaminifu kupeleka Injili ya marejeo ya Yesu. Mwenyekiti wa NTUC, Mch. Mark W. Malekana alihutubia waumini akihimiza kila mshiriki kutumika kwa uaminifu na kujitoa kikamilifu kwa wito tulioitiwa kama waasisi wetu wa Imani walivyojitoa maisha yao katika hali zote kumtumikia Bwana.



*Picha 15: Sherehe za Jubilee kutimiza miaka 150 ya utume iliyofanyika Bupandagila.*

## UKUAJI WA KANISA NA MALEZI YA WASHIRIKI:

Taarifa hii ni mwitikio wa kila mshiriki kutekeleza kauli mbiu isemayo Nitakwenda - Kuwafanya watu kuwa Wanafunzi wa Yesu Kristo. Kutokana na maazimio ya kuongeza idadi ya washiriki kubatiza watu 71,000 ikiwa ni goli la Conference. Baada ya mahubiri kufanyika muhula huu, watu **55,906 walibatizwa, sawa na 79% kufikia goli la ubatizo la Conference.**

**Jedwali hapa chini linaonesha ukuaji wa Kanisa kuanzia Robo ya 3 - Sept. 2022 hadi kufikia Robo ya 2 - Juni 2025 kwa kifupi.**

| Idadi ya washiriki Kabla ya Kugawa Conference | | | | Baada ya kugawa Conference |
|---|---|---|---|---|
| | ***Tulianza Robo ya 3, 2022 na*** | ***Kufikia Robo ya 2, 2025 ni*** | ***% Ongezeko*** | ***Tunabakia na*** |
| Makundi | 325 | 329 | 1.2% | 105 |
| Makanisa | 647 | 763 | 18% | 291 |
| Mitaa | 78 | 96 | 24.4% | 45 |
| Washiriki | 168,252 | 212,530 | 26% | 90,094 |

### *Malezi ya Washiriki:*

Semina za malezi ya washiriki zimetolewa na Katibu Mkuu wa Union ya NTUC, Mch. Magulilo Mwakalonge na Katibu Mkuu wa SNC, Mch. Onesmo Daniel wakiseminisha mabaraza ya Kanisa kuhusu **Malezi ya Washiriki** kwa kuziba mianya ya upotevu wa waumini wapya na kuhakikisha wanatoa

malezi bora katika kuimarisha imani zao na wanabaki Kanisani. Baada ya semina za urejeshaji kufanyika washiriki 1,709 walirejeshwa na kubatizwa (Re-baptized) kwa mujibu wa taarifa ya takwimu za washiriki SNC Sept. 22 hadi Jun. 2025.

## RASILIMALI FEDHA

Tunamshukuru Mungu kwa kazi njema iliyofanywa katika Conference yetu kupitia Idara ya Uwakili. Tunawashukuru waumini pia, kushiriki mibaraka ya Bwana kwa kutoa mali, kuwa tayari kutumia karama, muda, na mivuto yao kuwezesha kazi yake Yeye aliyetutuma ambayo imefanyika kwa ufanisi mkubwa.

Hali ya matoleo ya Zaka, Sadaka na Sadaka ya Makambi muhula huu ni kama ifuatavyo:

| *Matoleo* | *Zaka* | *Sadaka* | *Makambi* |
|---|---:|---:|---:|
| 2023 | 4,861,044,477.39 | 1,910,297,159.47 | 429,270,633.46 |
| 2024 | 5,909,098,223.66 | 2,355,410,112.09 | 489,375,133.33 |
| 2025 (Jan – Ago) | 3,445,558,124.26 | 1,403,947,852.95 | 323,962,095.51 |
| ***Jumla*** | ***14,215,700,825.31*** | ***5,669,655,124.51*** | ***1,242,607,862.3*** |

Idara ya Uwakili imetoa semina za uamsho wa Uwakili katika makanisa, mitaa na Kanda ni pamoja na majuma ya maombi ya Uwakili yaliyoendeshwa na walei, wachungaji, wakurugenzi wa Idara toka ngazi ya Division, Union na Conference.

Idara ya Uwakili kwa kushirikiana na Ofisi ya Hazina na Idara ya Mawasiliano walifanikiwa kufikia baadhi ya makanisa na mitaa kutoa semina juu ya utunzaji wa mali za Kanisa kwa kutumia mfumo wa Adventist Church Operations System (ACOS) mfumo ulioanza kutumika Machi 2024.

GCAS wamefanya ukaguzi South Nyanza Conference tumepokea Hati safi ya ukaguzi katika muhula huu.



*Picha 16: Ofisi ya Hazina wakitoa semina ya ACOS kwa mitaa SNC.*

## KITENGO CHA ATAPE:

Kitengo cha ATAPE Conference ambao ni wajasiriamali na wanataaluma waliojitoa kumtumikia Bwana kwa mali na karama zao kupeleka injili ya milele kwa kasi. Tunamshukuru Mungu kwa Wana ATAPE ambao wamechangia asilimia kubwa kuendesha mikutano ya injili ijulikanayo Net Event kwa kutumia mali na taaluma zao kutoa huduma za kiafya na kujenga makanisa.

ATAPE Mwanza kwa ushirikiano na Idara ya Huduma za Familia SNC waliendesha mahubiri ya Maisha ya Familia katika kituo cha High Profile, Mwanza Hotel. Mahubiri haya yalizaa matokeo chanya na kuanzisha Kituo cha mvuto chenye lengo la uinjilisti ili kuwafikia watu wa daraja la juu jijini Mwanza.

Kila mwaka ATAPE wamekuwa na Retreat zilizofanyika ili kupata semina kwa wajasiriamali na wanataaluma na kuweka mipango kwa ajili ya maendeleo ya chama na utume. Bwana awabariki kwa moyo wa ukarimu kwa kujitoa kwenu.



*Picha 17: Kamati ya wana ATAPE katika mahubiri ya Maisha ya Familia na wakiwa na Mhubiri, Mkurugenzi wa Huduma za Familia ECD, Dr. Winifrida Mitekaro.*

## UJENZI WA OFISI YA MAKAO MAKUU YA CONFERENCE MWANANCHI.

Mipango ya ujenzi ilianza mwaka 2020 na Mei 22, 2022 tulizindua ujenzi kwa kukata ardhi (Ground Breaking) katika viwanja vya Mwananchi wilayani Nyamagana. Tunamshukuru Mungu mpaka sasa ametuwezesha kufikia hatua ya kuweka slab ya kufunika basement ambayo imeshamwagwa, nguzo za ghorofa ya chini zimekamilika, ngazi anzilishi na njia ya wenye mahitaji maalumu zimekamilika. Kwa neema ya Mungu ni matumaini yetu ifikapo mwishoni mwa mwaka 2025 Desemba Slab ya ghorofa ya Kwanza iwe imekamilika.



*Picha 18: Ujenzi wa Ofisi Mpya ukiendelea katika eneo la Mwananchi.*

## KUBADIRI TASWIRA YA CONFERENCE

### *Ujenzi wa Nyumba za Wachungaji.*

Tunawapongeza washiriki na Wachungaji wa mitaa kuendeleza wazo la ujenzi wa nyumba za wachungaji. Tunaishukuru Kamati ya ujenzi wa nyumba za wachungaji katika kuhamasisha na kutia moyo mitaa kujenga nyumba za wachungaji na majengo mengine ya mitaa. Lengo la Conference kila Mtaa kuwa na nyumba ya Mchungaji na ndio sababu ya kuunda kamati.

Hadi sasa nyumba za wachungaji zilizojengwa na zinazotumika ni 49 kati ya hizo 15 zipo SNC na 34 zipo SRF na ambazo zinaendelea na ujenzi mpaka sasa ni nyumba 37 kati ya hizo 18 zipo SNC na 19 zipo SRF. Ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Conference ilisaidia ukarabati kwa nyumba 23 za watumishi, zilizoko mitaani na zilizoko katika ofisi kuu ya conference.


*Picha 19: Kamati ya ujenzi wa Nyumba za Wachungaji wakiwa katika Nyumba ya Mchungaji wa Mtaa.*

## *Ujenzi wa Makanisa:*

Lengo la Conference ni kuhakikisha makanisa ambayo yalikuwa hayajakamilika kujengwa, yanakamilishwa na injili inapoingia maeneo mapya makanisa yanajengwa. Makanisa Mapya 127 yanaendelea kujengwa kuanzia 2022 hadi 2025 na yako katika hatua tofautitofauti za ujenzi.


*Picha 20: Jengo la Kanisa la Waadventista wa Sabato Buzuruga ambalo ujenzi wake unaendelea.*

*Kuweka Wakifu Makanisa:*

Makanisa yaliyowekwa wakfu na Mwenyekiti SNC, Mch. Beatus Mlozi ni Kanisa la Mwamanyili, mtaa wa Masanzakona na Kanisa la Ikungulipu. Kanisa la Kirumba liliwekwa wakfu na Mwenyekiti wa ECD, Dr. Mch. Blasious M. Ruguri May 12, 2025.



*Picha 21: Mwenyekiti wa Division ya ECD Dr. na Mch. Blasious M. Ruguri mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe.Said Mtanda.*

## HUDUMA ZA KICHUNGAJI

Kufikia June 2025 jumla ya wachungaji waliokuwa kazini ni 114, na wachungaji wastaafu ni 10. Wachungaji waliowekewa mikono muhula huu ni 8. Hivyo, jumla ya wachungaji wote waliowekewa mikono ambao wako kazini ni 45.



*Picha 22: Wachungaji waliowekewa mikono katika Kanisa la Waadventista wa Sabato Januari 2024.*

Huduma za wachungaji mitaani: Uwiano wa Mchungaji mmoja anahudumia washiriki 2,191 na Mchungaji mmoja anahudumia makanisa 8. Uwiano huu unaonesha kuwa tunahitaji wachungaji zaidi ili kuhudumia waumini kwa ukaribu zaidi.

Wachungaji shujaa wawili wakiwa katika utumishi wao walilala mauti na Mchungaji mmoja mstaafu alilala mauti.

Baada ya kugawanywa Conference, SNC tumebakia na wachungaji walioko kazini 56, wachungaji waliowekewa mikono 26 ambao wako kazini na wachungaji wastaafu 4.

### *Huduma za Chama cha Wenzi wa Wachungaji*

Tunashukuru timu yote ya uongozi wa wenzi za Wachungaji katika huduma yao ya kuwatembelea na kutia moyo familia za wachungaji wastaafu, wajane na walio kazini katika swala zima la utume wa Kanisa.

Wenzi wa wachungaji waliokuwa kazini ni 106, wastaafu 8, Wajane, 19. Jumla ya wenzi wa Wachungaji wote kabla ya kugawanywa field Mpya ya Simiyu River Field walikuwa 133 na waliobaki SNC baada ya kugawanywa ni 64.



*Picha 23: uongozi wa Wenzi za Wachungaji kutembelea familia za kichungaji.*

### *Huduma za Uamsho na Matengenezo:*

Huduma hii imefanyika makanisani na kupokelewa na waumini mwaka hata mwaka kwa mafanikio makubwa. Wajumbe 179 walihudhuria Semina ya ECD iliyofanyika Singida May 17-25, 2024 ya Kurejea Madhabahuni na kuundwa Kamati ya Maombi ya Conference.

## HUDUMA ZA FAMILIA

Mahubiri ya Maisha ya Familia yakiwa ni program ya ECD Evangelistic Impact 2025 yalifanyika katika Conference yote tukiwa na vituo 734, watu 6196 walibatizwa. Jijini Mwanza March 17 hadi April 13 2024 Mkurugenzi wa Huduma za Familia ECD, Dkt. Winfrida Mitekaro aliendesha mahubiri ya Maisha ya Familia (Family life) katika kituo cha New Mwanza Hotel kwa kusudi la kuwafikia watu wa daraja la juu (High Profile). Ikiwa ni matokeo ya mahubiri haya kituo cha mvuto Mwanza New Life Center kimeanzishwa kuifikia jamii hii na kwa kusudi la kufikisha injili kwa wote.

Semina maalumu za malezi ya mtoto wa kiume zilizozinduliwa na Mwenyekiti wa SNC Pr. Beatus Mlozi, March 27, 2025 mkoani Simiyu katika Kanisa la Bariadi, na semina hizi kufanyika mkoani Mwanza Kanisa la Pasiansi na Kanisa la Misungwi. Wajumbe 696 walipata mafunzo ya semina hii.



*Picha 24: Dkt. Frida Mitekaro akiendesha mahubiri ya Famili life kituo cha High Profile Mwanza Hotel.*

## UINJILISTI KWA NJIA YA VITABU:

Team ya wainjilisti wa vitabu kufikia June 2025 jumla yao walikuwa 267, kati ya hao wakiwemo Cheti cha III na cha II Wainjilisti 43. Baada ya kugawanywa Conference tumebakiwa na team ya wainjilisti wapatao 117, wakiwemo Cheti cha III na II Wainjilisti 30.

Idadi ya vitabu vilivyouzwa muhula huu ni 226,590. vyenye thamani ya Tsh. 1,749,523,404.

**Kitabu cha Pambano Kuu** kilizinduliwa rasmi March 5, 2023 na Mwenyekiti SNC, Mch. Beatus G. Mlozi, katika Kanisa la Kirumba; zaidi ya watu 2000 walihudhuria. Katika tukio hilo tulikuwa na OCD mgeni wa Serikali. Kupitia michango toka makanisani na watu binafsi vitabu vya Pambano Kuu 1,700. viligawanywa kwa wasio waumini wa Kanisa.




Mwenyekiti wa Conference alizindua Jarida la Kimulimuli la Idara ya Uchapaji South Nyanza Conference May 31, 2024, ambapo nakala 220 zilitolewa siku hiyo.




Wainjilisti na wajumbe toka makanisa ya Conference 183 walihudhuria semina ya Roho ya Unabii Bariadi Oktoba 8-12, 2024 iliyoendeshwa na viongozi wa Idara toka NTUC Pr. Joseph Lusega, HHES Pr. Mdojano S. Msilikale na Pr. Daudi Benjamini.

## HUDUMA ZA AFYA NA KIASI:

Tunamshukuru Mungu kwa Idara hii ambayo imekuwa ikitoa elimu ya afya na kiasi na huduma za kiafya kwa jamii kupitia Hospitali. Tunawashukuru na kuwapongeza watumishi wote wa SDA Pasiansi Hospital kwa kuwa tayari kutumia karama zao kwa moyo wa upendo, huruma na kujali wagonjwa na kuwapa matumaini katika huduma zao; huduma ambayo ni mkono wa kuume wa injili, kile alichofanya Yesu alipohudumia wagonjwa hapa duniani. Bwana awabariki. Kupitia huduma hii watu 647 wamebatizwa.

Dkt. Ted Wilson aliweka wakfu Pasiansi Adventist Hospital, Februari 2, 2023 akiwataka watumishi kufanya kazi kwa bidii na kutoa huduma kwa wagonjwa na kuwatia moyo na kuwasaidia kiafya, kimwili, kiakili na kiroho katika swala zima la kuokoa Maisha ya wagonjwa ikiwa ndiyo jukumu la Kanisa kwa jamii.



*Picha 25: Dkt Ted Wilson akiweka wakfu Hospitali ya Waadventist Pasiansi*

Kongamano la Afya lililofanyika Agosti 14-17, 2023 Mwanza Kanisani Pasiansi likiendeshwa na Mkurugenzi wa Afya na Kiasi GC, Dr. Peter Landless na Dr. Zeno Marcel na Mkurugenzi wa Afya na Kiasi Union Dr. Kabhele; walielimisha waumini kuhusu elimu ya Mtindo wa Maisha ya Mkristo.



Tumeongeza vifaa vipya kwa ajili ya ufanisi mzuri wa kazi kwa Hospitali ya SDA Pasiansi ambavyo ni Full Blood Picture Machine na Digital X-Ray Machine.

Watumishi 10 wa Hospitali walishiriki kutoa huduma za Afya katika mahubiri ya Net Event Kahama na mahubiri ya Isangijo mtaa wa Kisesa.

Hospitali ya SDA Pasiansi walishiriki Siku ya Figo duniani Machi 13-14, 2025 wakishirikiana na Shirika la Africa Healthcare Network, watu 337 walihudumiwa. Sambamba na huduma hiyo Machi 16-22, 2025 Hospitali iliweka kambi la kupima afya bure, watu toka ndani na nje ya Mwanza 2,273 walihudumiwa.

## HUDUMA ZA VIJANA

Tunamshukuru Mungu kwa Huduma za vijana SNC kujitoa kikamilifu kumtumikia Bwana kwa moyo. Matendo ya vijana yameshika kasi katika muhula huu kuifikia jamii inayowazunguka kwa mafanikio makubwa. Tunawashukuru washiriki wote katika makanisa mahalia kushikamana na vijana katika huduma hii, hebu roho hii na iendelee ya kuwaelekeza na kuwarithisha vijana wetu utume wa Kanisa.



Idara imekuwa na makambi ya Conference kule Busulwa na Ngulyati na kambi la Union kule Guta - Bunda. Jumla ya Master Guides waliohitimishwa ni 260 na SYL 66.

Chama cha Watafuta Njia waliohitimu madarasa yao na kupata vyeti na pini ni 8,836 pamoja na Nishani walizotunukiwa zikiwa 12,401. Chama cha Wavumbuzi waliohitimishwa madarasa ni 6,910 na tuzo ni 9,783. Chama cha Mabalozi waliopata vyeti nya Moduli ni 4,003, na waliopata pini baada ya kumaliza moduli zote ni Mabalozi 103.

Huduma katika Kampasi za umma (PCM), vijana wa ASSA wapatao 32,400 na TUCASA wapatao 1,837 katika Conference yetu, wamekuwa na mikutano yao ya kila mwaka iliyofanyika kwa ufanisi mkubwa. Kupitia mikutano hii vijana wana ASSA 625 walibatizwa.

Vijana wamefundishwa masomo ya unabii, mahusiano, masomo ya ujasiliamali, moduli za Chama cha Mabalozi, mafundisho ya uongozi kuwaandaa kuwa viongozi bora, mafunzo ya muziki, elimu ya Mtindo wa Maisha na usafi wa maisha katika mikutano hiyo.

Vijana wa PCM wameshiriki katika Mpango wa EEI 2025 kwa kufanya Mahubiri, ambapo vijana wa ASSA walikuwa na vituo 32 vya mahubiri watu 2,003 walibatizwa na TUCASA walikuwa na vituo 22 ndani na nje ya Conference kama vile Bunda, Ukerewe na Geita, watu 1,683 walibatizwa.

Kupitia huduma za vijana katika kushiriki mpango wa EEI wameongeza idadi ya washiriki kwa kubatiza watu 14,521.

## HUDUMA ZA CHAPLENSIA

Huduma za Chaplensia hutolewa katika magereza na Hospitali. Huduma za kiroho na mahitaji ya kimwili zimetolewa katika hospitali na magereza SNC, na wafungwa 106 wamebatizwa.



*Picha 26: Gereza la Malya mkoani Simiyu ni mojawapo ya gereza waliopata huduma*

## HUDUMA YA MAWASILIANO

Idara ya Mawasiliano imejikita katika kujenga madaraja ya matumaini na kuongeza wafuasi katika majukwaa yetu yote ya mitandao ya kijamii (facebook, instagram, youtube n.k) tumefikia 90% ya malengo tuliyo jiwekea kwa muhula huu.

Semina jumuishi za idara ya mawasiliano zimefanyika katika kanda mbalimbali za Conference zikisisitiza utendaji wa kazi katika Idara, namna ya kuandaa maudhui ya kimtandao na kuwafikia wengi, kutunza utambulisho (identity) wa Kanisa, na kurusha vipindi mbashara kupitia Hope Channel, youtube n.k.

Kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu Mkuu washiriki wetu wameingizwa katika mfumo wa ACMS na kuboresha matumizi ya mfumo wa Adventist Church Operations System (ACOS) wakishirikiana na ofisi ya Hazina na Idara ya Uwakili ambapo hadi Juni 2025 washirkiki 178,000 tayari walikua wameshaingizwa.



## HUDUMA ZA WANAWAKE

*Idara ya Wanawake katika Utume wa Kanisa:*

Idara ya Wanawake imefanya semina zake katika Kanda, Mitaa na kufikia baadhi ya makanisa mahalia, pia wamekuwa na makongamano ya Kikanda katika Conference, na Kongamano la Union lilofanyika Nyegezi 2023 pamoja na Kongamano la ECD liliofanyika Ititi – Singida 2024.

Huduma kwa jamii zimetolewa na kufanya mahubiri ya hadhara watu 1,977 walibatizwa.

Kwa umoja wao wamejenga Kanisa la Buyubi mtaa wa Nyalikungu. Wamenunua viwanja wilayani Magu katika Kijiji cha Kisamba heka 1, na Kisesa-Ihushi eneo la heka 11.2, na Kijiji cha Ichobela heka 2 pamoja na kiwanja katika Kijiji cha Gamboshi – Bugabu, wilayani Bariadi ¾ ya heka. Wanawake ni jeshi kubwa, Bwana awabariki katika kujitoa kwenu kwa hali na mali.



*Picha 27: Kanisa la Buyubi Mtaa wa Nyalikungu lililojengwa na Wana wa Kike SNC 2023.*

## HUDUMA ZA WATOTO

Semina za Idara ya watoto kwa walimu zimefanyika kwa baadhi ya mitaa na Kanda katika Conference yetu, na kuhudhuria mikutano iliyoandaliwa na Idara ya Watoto ECD na NTUC. Walimu wamepewa mafunzo maalumu kuwasaidia watoto kukua kiroho, kimwili, kiakili na kijamii.

Makongamano kwa Idara ya Watoto Conference katika makanisa, mitaa na Kanda yamefanyika kwa kusudi la kuwasaidia watoto kutumia vipaji na karama zao kwa ajili ya kumtumikia Mungu na kuwasaidia wao binafsi katika maisha yao ya kiroho, kimwili, kiakili na kijamii.

Mahubiri ya watoto program ya ECD Evangelistic Impact 2025 na mikutano ya makambi iliyofanyika roho 1052 zilibatizwa.

## HUDUMA YA ELIMU

SNC tumekuwa tukihudumia Taasisi tano za elimu nazo ni: - Shule za Sekondari tatu ambazo ni Bupandagila Adventist Secondary School, Ngulyati Secondary School na Nyanza Adventist Secondary, Shule ya Msingi

ni moja Bupandagila Adventist Primary School na Chuo kimoja cha Nyanza Adventist Vocation Training College (NAVTC).

Taasisi zetu za shule kwa ujumla hutoa huduma za kiroho sawa na utume wa Kanisa. Kupitia huduma ya uinjilisti roho 833 walijitoa kwa Yesu na kubatizwa.

Tumefanikiwa kutembelea Taasisi za elimu na kuendesha semina mbalimbali kwa watumishi na kufanya vikao katika kuboresha huduma za taasisi mahalia.

Semina za Idara ya Elimu zimetolewa katika makanisa na mitaa na nyakati za makambi kuelimisha waumini kuhusu umuhimu wa Elimu ya Ki-Adventisti inayotolewa katika shule zetu ni pamoja na makanisa mahalia kuhakikisha vipindi vya dini katika shule za serikali wanafunzi wanahudumiwa na kutumia mtaala wa vipindi vya dini.

Katika muhula huu Taasisi zetu kwa ujumla katika swala la elimu wamefanya vizuri, upande wa sekondari kufikia ufaulu wa kufuta division 4 na 0. Wanafunzi wa Darasa la Saba wao wamefaulu kwa kiwango cha alama A na B, na upande wa Chuo cha NAVTC wanafunzi waliohitimu Muhula huu wa miaka mitatu kwa ujumla wake katika fani zao ni wahitimu 94.



Upanuzi wa maeneo ya Taasisi za Kanisa: Bupandagila Adventist Primary School wamenunua eneo lenye ukubwa wa heka tano. Ngulyati Sekondary wamenunua eneo la ukubwa wa heka tatu.

Taswira za Shule:  Bupandagila Sekondary kufanya ukarabati wa majengo na kupaka rangi, Nyanza Adventist Secondary kuwekewa madirisha ya vioo kwenye madarasa na kupaka rangi majengo, Ngulyati Sekondary kuweka madirisha ya aluminium kwa mabweni yote na BAPS wanajenga bweni la wavulana na wamepaka rangi majengo ya shule.

Baada ya kugawanywa kwa Conference tuna Taasisi mbili za elimu, Nyanza Adventist Secondary School na Chuo cha NAVTC.



*Picha 28: Bweni la Wasichana katika Shule ya Sekondari Ngulyati.*

## MIPANGO MBELE YETU.

1. Kutekeleza Agizo la utume: na kauli mbiu isemayo “Yesu anakuja, Nitakwenda”
2. Kufundisha uongozi wa Kikristo na kuwaongoza katika utumishi.
3. Kusukuma uinjilisti kwa njia zote muhimu na kuingia maeneo mapya.
4. Malezi na utunzaji wa washiriki wetu.
5. Kuhakikisha mitaa yote inatumia mfumo mpya wa Adventist Church Oparating System (ACOS)
6. Kuhakikisha ujenzi wa Ofisi ya Conference unamalizika.
7. Kuhakikisha kila mtaa, Kanisa na Taasisi zetu zinajishughulisha na mabadiliko ya taswira (Image changes).